BENKI MAZAO

Mchakato, Matokeo na Mabadiliko katika Jamii

Uzoefu kutoka Dodoma na maeneo mengine nchini

BENKI MAZAO
Mchakato, Matokeo na Mabadiliko katika Jamii

Kitabu hiki kimetayarishwa na:
Baruani Iddi kwa niaba ya PELUM Tanzania

Wahariri:
Donati Alex Senzia
Josephine Joseph Mkunda

© PELUM Tanzania 2012

ISBN 978 - 9987 - 8956 - 7 - 0

Kimepigwa chapa na:
Ecoprint Ltd,
S.L.P. 65182,
Dar es Salaam
Tanzania
Barua Pepe: ecoprinttz@yahoo.com

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Mratibu,
PELUM Tanzania
S.L.P 390, Morogoro-Tanzania
Simu/Nukushi: +255 23 2613677
Barua pepe: info@pelumtanzania.org
Tovuti: www.pelumtanzania.org

YALIYOMO

Ukurasa

Utangulizi v

Sehemu ya Kwanza 1
Chimbuko la Benki Mazao
Benki Mazao ni nini?
Kwa nini Benki Mazao katika maeneo ya wakulima wadogo?
Sehemu ya Pili 9
Mchakato wa uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa Benki Mazao
Hatua ya kwanza 9
Uhamasishaji wa jamii katika uundwaji wa jumuiya za uhakika wa chakula
Hatua ya pili 11
Mafunzo ya kuzijengea uwezo jumuiya za uhakika wa chakula
Hatua ya tatu 13
Uongozi na usimamizi wa Benki Mazao – wajibu na majukumu
Hatua ya nne 13
Makubaliano ya kuanzishwa kwa akiba za aina mbalimbali na mifuko ya mzunguko
Hatua ya tano 16
Uamuzi wa kuwa na sehemu ya hifadhi ya nafaka au mazao
Hatua ya sita 18
Uamuzi wa kuanzishwa kwa mfuko wa jamii ndani ya benki mazao
Sehemu ya Tatu 19
Jinsi Benki Mazao zinavyofanya kazi [Utendaji na Usimamizi]
Sehemu ya Nne 25
Matokeo chanya ya uanzishwaji wa Benki Mazao: Uzoefu kutoka Tarafa ya Chilonwa, Dodoma
Sehemu ya Tano 27
Changamoto za uendeshaji na usimamizi wa Benki Mazao
Sehemu ya Sita 29
Uendelevu wa Benki Mazao

UTANGULIZI

PELUM Tanzania ni mtandao wa Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali yanayofanya kazi na wakulima na wafugaji wadogo nchini Tanzania. Wanachama hawa wamejumuika pamoja ili kuwezesha kujifunza, kutandaa pamoja na ushawishi na utetezi kwa ajili ya kilimo endelevu.

Kazi kuu ya PELUM Tanzania ni kuhamasisha na kuendeleza kilimo endelevu kwa njia ya kujenga uwezo wa Mashirika Wanachama; kutandaa; kutunza na kueneza habari; na ushawishi na utetezi. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995, taasisi hii imekuwa ikifanya kazi bega kwa bega na wanachama wake katika maeneo mbali mbali nchini ikiwa na dhamira ya kuchangia ndoto ya taifa katika kuboresha maisha na ustawi wa wananchi kupitia kilimo endelevu.

Baadhi ya maeneo ambayo PELUM Tanzania inafanya kazi ni mikoa iliyoko katika kanda ya kati, moja ya mikoa hiyo ni Dodoma. Miongoni mwa shughuli ambazo wanachama wa PELUM Tanzania katika mkoa huu wamekuwa wakizifanyia kazi ni kuwezesha wakulima wadogo katika kuhakikisha kuwa wana "Uhakika wa Chakula" angalau katika ngazi za kaya. Hii inatokana na athari mbaya zinazotokana na familia nyingi za wakulima wadogo wadogo kutokuwa na uhakika wa chakula kwa vipindi fulani vya mwaka vinavyojirudia.

Mtawanyiko wa mvua usiolingana wa kimazingira na hali ya hewa umekuwa na athari tofauti katika maeneo mbali mbali ya nchi hii. Tofauti hizi za kimazingira kwa ujumla zinachangia kuwepo kwa tofauti za mitindo ya kimaisha na ustawi katika jamii husika.

Mikoa iliyopo katika kanda ya kati, Dodoma ikiwa mojawapo, imekuwa ikukumbwa na gharika au athari za upungufu wa chakula kwa vipindi visivyopungua miezi mitatu hadi minne vya kila mwaka. Baadhi ya sababu zinazotajwa kuchangia tatizo hili ni pamoja na upungufu wa mvua [kwa kuangalia kiasi/uwingi na mtawanyiko usio na uwiano – *Ukame na mara nyingine mafuriko*], mbinu duni

zitumiwazo na wakulima katika uzalishaji mazao ya chakula *k.m "kuberega",* huduma duni za ugani katika eneo la uzalishaji mazao, tatizo la pembejeo zikiwemo mbegu, upotevu wa chakula shambani na baada ya mavuno, kutokuwepo kwa mipango thabiti ya matumizi ya chakula katika ngazi za kaya n.k.

Kufuatia kero na athari mbaya za kujirudiarudia kwa matatizo ya upungufu wa chakula, wananchi wamekuwa wakifanya jitihada mbali mbali kupambana na tatizo hilo. Tatizo la upungufu wa chakula limekuwa sugu na linapunguza kwa kiasi kikubwa kasi ya maendeleo ya jamii husika na nchi kwa ujumla.

Uzoefu wa jitihada za kupambana na athari za upungufu wa chakula na matatizo ya njaa unaoelezwa katika kijitabu hiki, utajikita kwa sehemu kubwa maeneo ya mkoa wa Dodoma hususani katika tarafa ya Chilonwa. Lakini pia utahusisha uzoefu kutoka maeneo mengine ambayo yamejaribu kupambana na tatizo hili pamoja na mengine yanayohusu sekta ya uzalishaji na masoko ya mazao.

Tatizo la upungufu au ukosefu wa chakula katika maeneo mengi ya mkoa wa Dodoma limekuwa likijitokeza kwa kiwango kikubwa katika vipindi vya kati ya miezi mitatu mpaka minne kwa kila mwaka likisababishwa zaidi na upungufu wa mvua. Kufuatia tatizo hili, serikali na taasisi mbali mbali zimekuwa zikijikita katika kutoa misaada ya dharura hasa balaa la njaa linapojitokeza. Hatua hizi ni muhimu sana, lakini ni vema zikaangaliwa zaidi ya hapo na hasa suala la ufumbuzi endelevu.

"Katika maeneo ya mkoa wa Dodoma, baadhi ya matokeo yasiyoridhisha au kutia moyo yanayotokana na upungufu au ukosefu wa chakula ni pamoja na wanafamilia (hasa wanaume) kulazimika kufanya vibarua ili kupata chakula. Kwa kuwa tatizo hili hutokea katika msimu wa kilimo, vibarua hivi hupunguza sana nguvu kazi ya familia ambayo ingetumika katika kuzalisha mazao ya chakula. Matokeo yake ni uzalishaji mdogo na njaa au upungufu wa chakula katika msimu unaofuata".

Baadhi ya taasisi zinazojihusisha na maendeleo ya jamii katika maeneo ya Dodoma zilifanya tathmini na uchambuzi wa hali halisi ya maeneo zinayofanyia kazi kwa kuzingatia pamoja na maeneo mengine, tatizo la njaa au upungufu wa chakula. Taasisi MBILI za maendeleo ya jamii: INADES FORMATION Tanzania na LVIA (Lay Volunteers International) kwa kuzishirikisha jamii katika maeneo ya Kongwa na Chilonwa, ziliwezeshwa kuendesha mradi wa UHAKIKA WA CHAKULA kwa ufadhili wa shirika la INTERMON OXFAM.

"Mtazamo wa ujumla wa mradi huu wa uhakika wa chakula ulikuwa ni kuziwezesha jamii hizi kuwa na uhakika wa chakula (kwa wingi na ubora) katika kipindi cha mwaka mzima.

"Misingi mikubwa ya uwezeshaji ilibebwa na ukweli kwamba jamii hizi zimekuwa na uzalishaji duni wa mazao ya chakula, mbinu hafifu za kuhifadhi mazao, mifumo duni ya masoko ya mazao, mipango duni ya matumizi ya chakula katika ngazi za kaya na kutokuwa na mazao mbadala ya biashara kwa ajili ya kuongeza kipato, hivyo kulazimika kuuza mazao ya chakula ili kupata mahitaji yao mengine".

Ndugu mtumiaji wa kijitabu hiki, sehemu kubwa ya maelezo na mifano au rejea zilizomo ndani ya kijitabu hiki inahusu uzoefu na jitihada za wanajamii [hasa wale wa vijijini] kupunguza au kuondoa tatizo la upungufu, ukosefu au kutokuwa na uhakika wa chakula kwa kushirikiana na baadhi ya taasisi ambazo zilisaidia jamii hizo kwa njia za mafunzo na misaada ya fedha, vifaa au zana [hasa za kilimo, hifadhi au usindikaji].

Lengo la kijitabu hiki ni kutoa mwanga juu ya mbinu hii ya pamoja ambayo unaweza kuitumia kusaidia jamii yako au nyingine unayohusiana nayo kukabiliana na tatizo la kutokuwa na Uhakika wa Chakula. Vinginevyo, kijitabu hiki kinalenga kukupa hamasa ya **"kuthubutu"** kukabiliana na janga hili pindi linapojitokeza.

SEHEMU YA KWANZA
Chimbuko la Benki Mazao

Kwa tafsiri yoyote itakayotolewa leo hii, dhana hii imekuwepo tangu enzi za mababu zetu na tawala zao za kichifu au kitemi. Baadhi ya maeneo ya nchi leo hii unaweza kushuhudia maghala au vihenge vya kiasili vilivyotumika kwa malengo yanayoshabihiana na yale ya Benki Mazao zinazoanzishwa katika miaka ya hivi karibuni zikiwa na maboresho fulani fulani.

"Mkulima wa Kijiji cha Mbabala A Dodoma anakumbuka enzi za utawala wa watemi, *Kila kaya ilitakiwa kupeleka chakula kilichotunzwa chini ya usimamizi wa chifu/mtemi. Debe lilijazwa likiwa na ujazo wa zaidi ya kilo 20 [kisunzu/kishungi], lakini wakati wa kuchukua chakula hicho wakati wa upungufu, debe hilo hilo lilichukuliwa likiwa mfuto [bila kisunzu]. Kwa tafsiri ya leo, ile ziada [kisunzu/kishungi] ya debe ndiyo gharama za utunzaji au riba.*

Maghala ya nafaka wakati wa watemi

Vihenge vya asili Dodoma

Tatizo la ukosefu au upungufu wa chakula kwa vipindi vya kati ya miezi mitatu mpaka minne kila mwaka kwa maeneo ya wilaya za Kongwa na Chamwino – Dodoma lilisababisha wananchi kuweka mikakati mbalimbali ya kupunguza athari za tatizo hilo. Zifuatazo ni baadhi ya shuhuda zilizochangia kuanzishwa kwa Benki Mazao mkoani Dodoma.

Ushuhuda na 1: *Wanajamii katika tarafa ya Chilonwa wanakumbuka kipindi cha miaka ya 1997 – 1998 ambapo kulikuwa na janga la El nino ambapo mwananchi alilazimika kununua debe la mahindi kwa kiasi cha shilingi 4,000/=. Pamoja na jitihada nyinginezo, mbegu bora za Mtama na Uwele zilitolewa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya lakini mimea iliyoota ilishambuliwa na wadudu wajulikanao kama* ***"Makombelele"(Kigogo).*** *Njaa ilikuwa kali na wanaume kama kawaida walilazimika kuhama miji yao ili kutafuta vibarua ambavyo ujira wake ulikuwa fedha au chakula kidogo kisichotosheleza mahitaji ya kaya".*

Ushuhuda na 2*: "Katika miaka ya 1990 - 2000, wanajamii wa maeneo ya kijiji cha Chitego waliweza kuzalisha kiwango cha kuridhisha cha mazao, lakini kutokana na wakulima kuhitaji kukidhi mahitaji muhimu ya kimaisha bado waliuza mahindi yao kwa wingi sana kwani bei zilikuwa chini mno. Hali hii ilichangia kwa kiasi kikubwa njaa kali iliyojitokeza kati ya 1998 – 1999, ambapo miezi ya Januari na Februari mwananchi alitakiwa kununua gunia la mahindi kwa kiwango cha hadi kufikia* ***Shilingi 25,000/=*** *au kukopeshwa* ***gunia moja*** *la mahindi na baadaye kulipa* ***magunia sita baada ya mavuno****. Kwa lugha ya Kigogo mikopo hii iliitwa* ***"Songoleda".***

Ushuhuda na 3: *Tatizo la njaa katika vipindi vinavyojirudiarudia ndani ya mwaka lilikuwa ni wimbo wa kawaida na kupewa majina tofauti kila eneo la nchi "Kwa mfano kule Masasi njaa ya aina huitwa FEBU sababu ni kwamba ilijitokeza zaidi katika mwezi Februari ya kila mwaka ambapo wananchi hutambua na kujiandaa".*

Ushuhuda na 4: *Pamoja na kuwa ni moja ya maeneo yaliyo na fursa ya uzalishaji wa uhakika, wakulima wa Mbozi-Mbeya hawataisahau njaa ya mwaka 1984, iliyosababisha taasisi 3 [VECO Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na ADP Mbozi] kuanzisha Programu ya kuongeza uzalishaji wa mazao hasa ya chakula.*

Ushuhuda 5: **Katika makala mojawapo ya gazeti la Tanzania Daima [25 Septemba 2007], mwandishi mmoja aliandika makala juu ya Benki Mazao *[uzoefu wa kanda ya ziwa]*. Sehemu ya maelezo yake yalikuwa:**

"Kipindi cha mavuno, wakulima wengi hupenda kuuza mazao yao kwa lengo la kujipatia fedha za kulipia gharama walizozitumia wakati wa kilimo na kununua vifaa vingine muhimu kwa familia, lakini kipindi hicho pia hukabiliwa na bei ndogo ya mazao sokoni

Katika mazingira hayo ni dhahiri anayeumia ni mkulima wakati walanguzi na wachuuzi wa mazao hayo wakifurahia bei ndogo wanayotoa na kuuza mazao hayo kwa bei nzuri baada ya kusindika au wakati kuna mahitaji makubwa ya mazao au nafaka hizo.

Wakulima wetu katika kipindi hiki hawana njia mbadala kwani matumizi ya maghala ya kienyeji ya kuhifadhia nafaka sasa hivi hayapo tena baada ya njia hiyo ya kuhifadhi nafaka kupitwa na wakati au kuachwa kutokana na upungufu unaoendelea wa mavuno kutokana na sababu mbali mbali, ikiwemo mabadiliko ya hali ya hewa.

Kwa kuwa sasa ni nadra kukuta kaya wenye ghala angalau moja vijijini, wakulima wamekuwa wakinunua magunia au mifuko ya plastiki kwa ajili ya kuhifadhi mazao yao kwa muda mfupi kabla ya kupelekwa sokoni ili kuepuka gharama ya ziada ya kununua mifuko mingi ambayo haitatumika katika kipindi kirefu. Hali hii imeongeza kuwaweka wakulima katika nafasi mbaya ya kulazimika kuuza mazao yao mara baada ya mavuno ili kuepuka majanga kama moto au kubunguliwa kwa mazao na wadudu wanaoharibu nafaka na hivyo kuharibu ubora wa mazao hayo kabla ya kufikishwa sokoni."

Haya ni baadhi ya matukio yaliyochangia wanajamii kupitia jitihada zao au kwa ushirikiano na mashirika au taasisi za maendeleo ya jamii kutafuta suluhisho la madhara mbalimbali yanayompata mkulima au mwanajamii kijijini ambaye kimsingi ndiye mzalishaji wa msingi anayetarajiwa kunufaika na matunda ya jasho lake.

Mbinu mbali mbali zilibuniwa katika hatua za awali zikilenga “uhakika wa chakula”, ‘Hifadhi ya mbegu” na “misaada kwa jamii hasa makundi maalumu”, japokuwa baadaye mtindo na mfumo huo huo ulitumika kama sehemu ya kumudu soko hasa kwa maeneo yanayozalisha mazao ya biashara. Hapa ndipo lilipozaliwa jina maarufu la “Benki Mazao”, ikimaanisha hifadhi ya mazao kwa ajili ya malengo yaliyotajwa hapo juu

Kwa hiyo Benki mazao ni nini?
Benki Mazao [nafaka] ni taasisi iliyo au isiyo rasmi inayohusisha jamii au kikundi ndani ya jamii katika kuendesha na kusimamia shughuli zake [k.m. kukusanya, kununua, kutunza na kugawa au kuuza nafaka husika].

Kwa nini Benki mazao?
Kimsingi Benki hizi huanzishwa [rejea uzoefu wa taasisi hizi katika maeneo ya Dodoma] kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chakula hasa katika kipindi cha upungufu na wakati mwingine ukosefu wa chakula [Uhakika wa chakula]. Hii ndiyo sababu ya msingi lakini haizuii aina nyingine za utunzaji wa nafaka kufanyika ndani ya taasisi hiyo. Kutegemeana na mazingira, ni jukumu la wanajamii kuamua ni aina gani ya nafaka inayofaa kutunzwa ili kukidhi mahitaji wakati wa upungufu.

Angalizo: Benki Mazao zisichukuliwe kama mwokozi wa njaa, hii itasababisha kuwepo kwa dhana ya utegemezi kwa baadhi ya wanajamii. Badala yake Benki Mazao zichukuliwe kama mkakati wa pamoja ndani ya jamii ili kuhakikisha “Uhakika wa chakula” katika maeneo yao hasa yale ya vijijini.

Uhalali wa kuwepo kwa Benki Mazao zinazosimamiwa na wanajamii:
Benki Mazao kwa mfumo wa kusimamiwa na kuendeshwa na wanajamii unatoa majibu kwa matatizo na athari ya ukosefu au upungufu wa chakula kwa sababu zifuatazo:-

- Ni mfumo rahisi [katika usimamizi na uendeshaji];
- Huendeshwa na kusimamiwa na wanufaikaji wa mfumo huo [wanajamii];
- Huanzia katika ngazi za vitongoji/mitaa na hasa makundi yanayoathirika zaidi;
- Ni mfumo shirikishi – wanufaikaji kushiriki katika hatua zote za utoaji maamuzi;
- Haijengi utegemezi, badala yake huhimiza umiliki wa mchakato na matokeo ya uwepo wake;
- Gharama za uendeshaji au uanzishwaji kwa sehemu kubwa sana ziko ndani ya uwezo wa wanajamii;
- Ikiendeshwa kwa ufanisi hutoa suluhu ya kudumu ya tatizo la ukosefu/upungufu wa chakula [hasa kwa vile vipindi vya njaa vinavyojirudia rudia ukiondoa majanga ambayo ni vigumu kuyadhibiti k.m mabadiliko ya tabia nchi n.k].

Angalizo: Taasisi au chombo hiki kikisimamiwa ipasavyo [kuwa na mifumo thabiti, kuzingatia kanuni na miongozo n.k.], huhakikisha upatikanaji wa chakula katika vipindi vya upungufu au ukosefu wa chakula kwa jamii za wakulima hasa maeneo ya vijijini ambazo ni waathirika wa msingi na familia zao. Hii hupunguza adha ya kulazimu wakulima kufanya kazi za vibarua na hivyo kutotumia nguvu zao katika mashamba yao, kukimbia familia zao pamoja na athari nyingine za kijamii.

Mabadiliko au kupanuka kwa dhana ya Benki Mazao:
Ndugu msomaji, kwa vile Benki Mazao ni taasisi, basi nayo huangukia katika ukuaji na upanuaji wa shughuli nyingine kama zilivyo taasisi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni, Benki Mazao inaweza kubeba sura zifuatazo:

1. **Uhakika wa Chakula:** Hifadhi ya chakula kwa matumizi wakati wa upungufu au ukosefu wa chakula {Njaa};
2. **Uhakika wa Mbegu:** Hifadhi ya mbegu kwa kiwango bora kwa matumizi ya msimu unaofuata;
3. **Kumudu soko:** Mazao kutunzwa ili kusubiri wakati wa bei nzuri.

Hapa ndipo lilipo chimbuko la mfumo wa **"Mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani".**

Tofauti na **Benki Mazao kwa uhakika wa chakula na mbegu,** ambapo lengo kuu huwa ni kuboresha na kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha kutosha na bora katika vipindi vya upungufu au njaa kwa wakulima na familia zao. Mfumo wa **stakabadhi ya mazao ghalani** umejikita zaidi katika kuhakikisha soko lenye tija la mazao ya wakulima kwa kuhifadhi mazao mpaka kipindi cha bei nzuri ya mazao hayo. Hapa huhusisha pia utoaji wa mikopo kwa wanachama waliotunza mazao yao kama njia ya kujikimu ili kutolazimika kuuza mazao kwa bei ya chini.

Mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani unaimarika kwa nguzo zifuatazo:

i. Uhakika juu ya usalama wa mazao yaliyohifadhiwa
ii. Upatikanaji wa mikopo unarahisishwa
iii. Uwezo wa kutetea na kulinda bei ya mazao ni mkubwa
iv. Bei ya mazao isiyoyumba sana
v. Kudhibiti matumizi ya mazao hasa kipindi cha mavuno

Nguvu ya Mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, inatofautiana kwa kiasi fulani na mfumo unaolenga uhakika wa chakula. Changamoto zinazokabili mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani ni pamoja na:

a) Upatikanaji wa mikopo mara nyingi huwa katika muda tofauti na kipindi halisi cha mahitaji ya wakulima *mf. Mikopo kupatikana mwezi Julai badala ya Mei ambacho ni kipindi cha mavuno;*
b) Uanachama wa mfumo huu hubebwa zaidi na uwezo na upatikanaji wa mikopo na itokeapo vinginevyo, mfumo huu hukosa wanachama wa kutosha;
c) Mfumo huu unaweza kufanya vizuri hasa katika maeneo yenye uzalishaji wa uhakika wa mazao na hasa yale ya biashara *Mfano: Mpunga, Korosho, Kahawa n.k;*
d) Gharama za uendeshaji kwa nyakati tofauti huwa zikiongezeka, hivyo kupunguza mapato halisi anayopata mkulima mkononi.

***Mfano 1**: Gazeti moja la kiingereza liliandika makala iliyoelezea uzoefu wa mfumo huu katika mkoa wa Mtwara [Wilaya za Tandahimba, Mtwara vijijini, Newala, Masasi na Mtwara mjini] kwa zao la Korosho. Makala hiyo ilionesha kuwa bei anayolipwa mkulima ni Shilingi 700/= kwa kilo kwa mkupuo na si vinginevyo. Lakini lilichambua pia makato kama ifuatavyo: Kodi ya usalama/ulinzi, kodi ya taasisi na ushuru wa mazao [5%] kwa halmashauri vyote hivi kufikia Shilingi 106.50 kwa kilo. Pia gharama za masoko Shilingi 96/=; gharama za ununuzi Shilingi 39/= na gharama za mkopo Shilingi 18/=. Hii inafanya jumla ya makato kwa kilo ya korosho kufikia Shilingi 259.50. Kiasi hiki ni takribani asilimia 37 ya fedha yote ambayo mkulima angepata kwa malipo ya Shilingi 700/= kwa kilo.*

Mwanachi
Jumatano Mei 23 2012

'Stakabadhi ghalani sasa uondolewe'

Mwanja Iliadi, Masasi

WANANCHI wa Kijiji cha Mwenge Mtapika, Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara wameomba Serikali kuingalia upya mfumo wa kuondoa mfumo wa utaratibu wa mazao kwa njia ya stakabadhi ghalani wakidai kuwa mfumo huo unawaongezea umaskini wananchi, badala ya kuwakomboa kiuchumi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kijijini hapo na mwandishi wa habari hizi alipofanya ziara kujionea awamu ya pili ya korosho jinsi yanavyoendeshwa kwa wananchi.

Akizungumzia kwa niaba ya wananchi wenzake,Hadija Makoya alisema kuwa mfumo huo umesababisha maisha yao kuwa ya kuhangaika kwa vile yanategemea kilimo, hasa uuzaji wa mazao ikiwamo korosho.

Alidaiwa kuwa licha ya wakipanga kuuzamazao kwanjia ya stakabadhi ghalani,mfumo huo haujawaletea mabadiliko yoyote ya kiuchumi hali inayowapa ugumu wa maisha katika familia zao.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Evarist Kakolo alisema kuwa kupitia mfumo huo mwananchi amekuwa hawaruhusiki uza tofali akiamua Sh60 katika kila kilo anayouza Sh30 ni kwa ajili ya mfuko wa maendeleo na Sh30 kwa ajili ya pembejeo akidai kuwa pembejeo hizo hazifiki kwa wakati kama inavyotakiwa.

***Mfano 2**: Katika gazeti la Majira 23 Mei 2012, mwandishi ameainisha kuwa wakulima wa kijiji cha Mwenge Mtapika wilaya ya Masasi walionyesha kutoridhika na uendeshaji wa mfumo huo wa stakabadhi ya mazao ghalani. Katika moja ya kero walizozitoa ni ile ya kukatwa Shilingi 60/= kwa kila kilo ya korosho. Mchanganuo wa makato hayo ni Shilingi 30/= kwa ajili ya mfuko wa maendeleo na Shilingi 30/= kwa ajili ya pembejeo. Kero kuu ilikuwa ni ile ya pembejeo kutowafikia walengwa kwa muda muafaka japokuwa wamechangia.*

ANGALIZO: Kwa shuhuda mbili zilizotolewa hapo juu, haitoshi kuhukumu mtindo huu kuwa mbaya au haufai. Mara nyingi dhana inaweza kuwa nzuri na yenye tija isipokuwa uendeshaji, usimamizi, mifumo na taratibu ambazo mara nyingi hutengenezwa na wanachama au kushauriwa ndizo zinazoweza kwa kiwango kikubwa kupotosha mwelekeo chanya wa mfumo au mtindo husika.

SEHEMU YA PILI
MCHAKATO WA UANZISHAJI , UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA BENKI MAZAO

Uzoefu kutoka Dodoma na maeneo mengine kwa Benki Mazao zenye msingi mkuu wa uhakika wa chakula kwa wakulima na familia zao [hasa maeneo ya vijijini].

Hatua katika uanzishaji wa Benki Mazao kwa mtazamo wa awali wa kukidhi mahitaji ya chakula kwa familia za wananchi vijijini, unajikita katika mafunzo yaliyopatikana kutokana na mbinu za asili za kitanzania zikiwemo matumizi ya vihenge na maghala ya asili lakini pia mafunzo kutoka nje ya nchi yetu yaliyotumika kuboresha utekelezaji wa dhana hii.

Katika maeneo ya Dodoma, kuna uzoefu wa aina mbili katika uanzishwaji wa taasisi hizi. Kuna baadhi ya jamii kutokana na mahitaji yao walianza jitihada wao wenyewe na kuna baadhi ya maeneo au yalijifunza na kuanzisha yenyewe au yalihamasishwa kupitia taasisi za maendeleo zinazofanya kazi katika sehemu hizo. Mbinu zote za uanzishwaji wa taasisi hizi zinaweza kuwa zimepitia kwenye hatua zifuatazo:

HATUA YA KWANZA
UHAMASISHAJI WA JAMII KATIKA UUNDWAJI WA JUMUIYA ZA UHAKIKA WA CHAKULA

Ndugu mtumiaji wa kijitabu hiki, hakuna mwongozo maalumu wa uundwaji wa aina hii au inayofanana na hii ya taasisi za kijamii bali hutegemea zaidi mazingira na utashi wa jamii husika. Kinachoelezwa hapa chini ni uzoefu tu ambao unaweza kuboreshwa:

Uamuzi wa kuanzisha Benki Mazao

Uamuzi wa kuunda taasisi kama Benki Mazao ni lazima ujikite na uzingatie mahitaji, utashi na utayari wa jamii husika. Msukumo mkubwa uguse kiini cha tatizo litakalopelekea uanzishwaji wa taasisi hizo *k.m vile upungufu wa mazao na chakula katika vipindi virefu vya ukame*. Kwa vile utunzaji wa mazao utahusisha jamii, ni vema

majadiliano na makundi mbalimbali ndani ya kijiji yakapewa uzito stahili ili kuongeza ufahamu juu ya:

- Aina ya akiba
- Aina na kiasi cha nafaka
- Manufaa na taratibu za uendeshaji
- Wapi nafaka zitatunzwa n.k

Mikutano ya maafikiano baina ya makundi mbali mbali ndani ya jamii husika ni muhimu katika hatua hii tete ya mwanzo.

Uzoefu: *Ukiacha kijiji cha Chitego [ambacho juhudi zilianzia ndani ya jamii ya kijiji hicho kwa kuongozwa na sehemu ya wakeretwa wa masuala ya maendeleo ya jamii " Kikundi cha Nyota Njema"], Jamii katika maeneo ya tarafa ya Chilonwa [Dodoma] zilihamasishwa kuanzisha mifumo inayolingana na mazingira yao ikiwa ni pamoja na kuanzisha vikundi na mitandao ya kijamii iliyoendesha na kusimamia taasisi hizo.*

ZINGATIA:

Uamuzi wa kuanzisha Benki mazao ni LAZIMA utokane na maamuzi au UTASHI wa wanajamii wenyewe. Wakala au taasisi za nje ya jamii wasishinikize uanzishwaji wa taasisi kama Benki mazao. Jamii lazima iwe na umiliki kamili wa Benki mazao waliyoianzisha. Ushirikishwaji na demokrasia ni lazima zitumike katika kuchagua kamati itakayosimamia na kuendesha shughuli za Benki mazao kwa niaba ya wanachama au wanajamii. **"Taasisi au wataalamu toka nje wabakie kuwa washauri tu"** katika masuala ya ununuzi wa mazao/nafaka, utaalamu wa kuhifadhi, menejimenti ya ghala/stoo [sehemu ya kuhifadhia] na masuala ya masoko ya mazao au nafaka. Hii itapunguza **"utegemezi",** na hivyo kuifanya jamii husika kumiliki mchakato na manufaa ya Benki mazao na hivyo uendelevu wake.

MATOKEO KATIKA HATUA HII:

Kipindi fulani ***baada ya uhamasishaji, inatarajiwa kuwa kutatokea sehemu ya wanajamii watakaokuwa tayari kuanzisha umoja huo ikiwa ni pamoja na kuwa na uongozi wa muda au mpito.***

HATUA YA PILI
MAFUNZO YA KUVIJENGEA UWEZO VIKUNDI VYA UHAKIKA WA CHAKULA:

Majukumu yanayokabidhiwa kwa kamati za Benki Mazao baadhi yake yanahitaji mafunzo *k.m Mtunza hazina ni lazima awe na stadi au ujuzi angalau ule wa msingi wa utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu [Siyo lazima awe mtaalamu]*. Kwa hiyo ni vema kuwa na wanachama wenye sifa au waliotayari kujifunza. Lakini pia inawezekana kupata mtu wa nje kama juhudi za ndani zimeshindikana akiwa anawajibika kwa kamati husika.

Uzoefu: Vikundi wanachama vilivyobeba dhamana ya kuendesha na kusimamia Benki Mazao katika vijiji vya Chitego, Mgunga, Mlebe, Mnase, Chinangali II, Makoja na Ikowa vilipatiwa mafunzo ya msingi ambayo yaligusa stadi zifuatazo:

a. Mbinu za kilimo bora ili kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao;
b. Hifadhi bora ya mazao ya kilimo na utunzaji wa maghala;
c. Miradi ya kiuchumi ndani ya vikundi;
d. Stadi za uongozi, uimarishaji vikundi, uundaji wa katiba na usajili wa vikundi;
e. Taratibu za usimamizi wa rasilimali ndani ya vikundi k.m. Mifuko ya mzunguko, Mkopo wa chakula kutoka hifadhi ya jamii, akiba na mikopo ya vikundi n.k.

ANGALIZO: *Kama inawezekana ni vema mafunzo ya awali yakahusisha wanachama wote waanzilishi. Hii husaidia kuwa na uelewa wa pamoja na kumilikisha taasisi kwa wanachama wote.*

Mafunzo kwa viongozi na wanachama wa Benki Mazao

Muundo ndani ya Benki Mazao

Kwa kawaida wanachama wa Benki Mazao ni wale wanaoimiliki *[Yeyote ndani ya jamii husika anayeheshimu na kubeba dhamana ya wazo na dhana ya Benki Mazao na ambaye ananufaika na kuwepo kwa Benki hiyo]*. Wanachama ndiyo wanatakiwa kujua na kuweka lengo au madhumuni ya kuwa na Benki Mazao; kuamua usimamizi na uendeshaji wake [*k.m. iwepo kwa ajili ya kuhudumia wanajamii au kibiashara*] na watahusika katika usimamizi wa shughuli zote za Benki Mazao. Wanachama kwa kawaida hukutana mwanzo na mwisho wa kila msimu.

Kamati ya utendaji ya Benki Mazao

Wanachama wa Benki Mazao watachagua kamati tendaji ambayo itakuwa na Mwenyekiti, Katibu, Mhazini, mtunza ghala na wanunuzi. Panaweza kuwa na manaibu kama itatokea kuna tatizo kwenye nafasi mojawapo. Baadhi ya majukumu ya kamati tendaji yanaweza kuwa pamoja na:

- Kusimamia shughuli za kila siku za Benki Mazao;
- Kushauri wanachama masuala yanayohusu uendelezaji wa Benki Mazao;
- Kuhakiki mali na shughuli za Benki Mazao kila mwaka;
- Kuwajibika na kujibu hoja za wanachama wa Benki Mazao.

MATOKEO KATIKA HATUA HII: Miongozo, kanuni na *katiba za Benki Mazao kuundwa, viongozi/kamati kuchaguliwa kwa mujibu wa katiba, uamuzi wa kuanza kuweka akiba za aina mbalimbali hupitishwa na uamuzi wa wapi na aina ya hifadhi huamuliwa.*

HATUA YA TATU
UONGOZI NA USIMAMIZI WA BENKI MAZAO – WAJIBU NA MAJUKUMU:

Kwa ujumla, wanachama kupitia mkutano mkuu ndio wanao miliki Benki na mkutano mkuu ndio unaowachagua Mwenyekiti, Katibu na Kamati ya uendeshaji. Kamati ya uendeshaji ina kamati ndogo tatu, kama zifuatazo:

KAMATI YA UTENDAJI:

Mwenyekiti na Katibu wa Benki ni wajumbe na huwajibika na shughuli za kila siku za Benki (isipokuwa utoaji wa mikopo). Ikiwa ni pamoja na Ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo, utunzaji wa kumbu kumbu za mahesabu ya kila siku, ukaguzi wa nafaka ndani ya Benki na manunuzi ya mazao. Kamati hii hukutana mara kwa mara.

KAMATI YA MIKOPO:

Kamati hii ina jukumu la kupitia, kuchunguza na kutathmini maombi ya mikopo kutoka kwa wanachama. Ni chombo pekee ambacho kinapitisha maombi ya mikopo ya wanachama wa benki.

KAMATI YA USIMAMIZI:

Hii inahusika na udhibiti wa ndani wa rasilimali. Inahakikisha kuwa rasilimali zote zinatumika na kutunzwa kwa umakini wa hali ya juu. Pia inafanya ufuatiliaji wa kamati zote na kupitia taarifa mbalimbali za mikutano/vikao vya kamati husika.

HATUA YA NNE
MAKUBALIANO YA KUANZISHWA KWA AKIBA ZA AINA MBALI MBALI NA MIFUKO YA MZUNGUKO:

Kutokana na uzoefu na kutegemea Benki Mazao imeanzishwa kwa mfumo upi, nafaka/mazao yanayotunzwa kwa ajili ya uhakika wa chakula yanawezekana kupatikana kwa njia zifuatazo:

- Michango/hisa au akiba kutoka kwa wanachama au wanajamii.
- Msaada au ruzuku toka nje ya wanachama au wanufaika wa Benki Mazao
- Mikopo itolewayo kwa Benki Mazao.

Njia hizi tatu zinaweza kusimama kila moja peke yake au kuchanganyika na hivyo kuchangia urahisi na utoaji huduma katika wigo mpana.

Mikopo

Kwa kutegemea mazingira ya uanzishwaji wa Benki hizi, mkopo unaweza kuwa fedha au mazao/nafaka au vyote. Mikopo ya fedha ndiyo ya kawaida sana na hutolewa kwa masharti tofauti tofauti. Inaweza kuwa ya muda mfupi, wa kati au mrefu ikiwa na riba au bila riba. Ni vema wanajamii au wanachama wa Benki Mazao wakafahamishwa kwa kina masharti yanayoandamana na mikopo hiyo.

Ruzuku, msaada au Zawadi

Zawadi au ruzuku inaweza kutolewa na taasisi au mtu wa nje. Mara nyingi hii hutumika kama mtaji wa mzunguko kuchangia kupanuka kwa mtaji na utoaji huduma wa Benki Mazao kwa vipindi vijavyo. Hii humaanisha, fedha inayopatikana kutokana na mauzo ya mazao/nafaka kwa msimu wa kwanza hutumika kununua mazao au nafaka ya msimu unaofuata. Kama Benki itaweza kuendesha ruzuku hii vizuri huwa hakuhitajiki msaada tena toka nje ya Benki.

Mwaka 2002, Programu ya Uhakika wa chakula kupitia ufadhili wa Intermon Oxfam, ilitoa ruzuku ya Mbegu, na madawa. Jumla ya wakulima 221 katika maeneo ya mradi waliweza kuhifadhi jumla ya magunia 1073 ya mbegu; wakulima 223 walitumia mbegu bora za nafaka [*Kwa angalau kiwango cha ekari moja kwa mkulima].* Pamoja na ruzuku hiyo ya mbegu na madawa, mwaka huo huo jumla ya vikundi vitano katika maeneo ya Chitego, Gairo na Mikese vilipatiwa jumla ya magunia 189 ya mahindi kama mtaji anzia kwenye Benki Mazao na shirika hilo hilo.

Mchango wa jamii

Katika baadhi ya maeneo, wanachama au jamii inaweza kuchangia kwa kuwa na shamba la pamoja na mazao yanapouzwa, fedha inayopatikana inawekezwa ndani ya Benki Mazao. Mazao mengine kama matunda na mbogamboga yanaweza kulimwa na kuuzwa kwa ajili ya kununulia nafaka/mazao yanayoweza kuhifadhiwa katika benki. Vinginevyo, mwanachama au mwanajamii mmoja mmoja au kaya inaweza kuchangia nafaka/mazao baada ya mavuno ya msimu husika.

Mtaji wa Fedha

Katika maeneo ambayo kuna uzalishaji mzuri na ziada ya nafaka au uzalishaji unaotosheleza mahitaji ya jamii, inaweza kuwa vema kuanza na mtaji wa Fedha. Hii itawezesha Benki Mazao kununua mazao au nafaka za wakulima kwa bei nzuri na kuna uwezekano wa Benki kununua nafaka ili kukidhi mahitaji ya wanachama au jamii husika. Katika maeneo ambayo uzalishaji hautoshelezi mahitaji ya wanachama au jamii husika, kuwa na mtaji wa fedha kunaweza kuwapatia wakulima bei nzuri ya mazao kuliko bei ya wafanya biashara. Njia hii ni nzuri lakini huhitaji kamati zilizo makini na uwezo kwa sababu kunakuwepo na ushindani wa ki masoko na wanunuzi wengine wa reja reja. Utata wa njia hii ni pamoja na usalama wa fedha [inaweza kulazimu kujua taratinbu za kibenki ikiwemo kufungua akaunti n.k. Athari nyingine ni kwamba, Benki inaweza kupatiwa kiwango kikubwa cha fedha na hivyo kushawishika kutumia katika masuala tofauti na hifadhi ya nafaka. Hapa mambo ya msingi kabla na baada ya kuanzishwa kwa mifuko ni:

- ✓ *Kufahamu kwa kina juu ya madhumuni ya kuanzisha na kuwepo kwa mifuko ya aina hii;*
- ✓ *Kufahamu jinsi ya kuisimamia na kuiendesha kwa ufanisi;*
- ✓ *Kuainisha na kutambua mafanikio yanayotarajiwa ili kufikia malengo maalum ya mfuko huu.*

Katika Programu ya Uhakika wa Chakula iliyoendeshwa katika Tarafa ya Chilonwa, Gairo na Mikese kupitia ufadhili wa Intermon Oxfam, mifuko hii ya mzunguko ilitolewa na mradi na kusimamiwa na vikundi baada ya mafunzo yaliyohusu uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Benki Mazao ikiwemo rasilimali fedha.

HATUA YA TANO
UAMUZI WA KUWA NA SEHEMU YA HIFADHI YA NAFAKA AU MAZAO:

Ghala

Ghala la kutunzia nafaka ni vema likajengwa mahali panapofikika na pana ulinzi wa kutosha. Jamii katika kijiji husika ihusishwe katika kuamua ni wapi ghala lijengwe, vifaa gani vitumike katika ujenzi? na je ni la muda au la kudumu? au la kukodishwa? au kuazimwa n.k.

Mambo ya kuangaliwa wakati wa kuchagua aina ya ghala

Ghala la muda [*sio la kudumu*] linaweza kujengwa na wanachama au wanakijiji wenyewe. Vifaa vya ujenzi vinaweza kupatikana ndani ya kijiji husika na huwa siyo la gharama kubwa au kuhitaji utaalamu mkubwa. Lakini izingatiwe hapa kuwa, halitakuwa imara na huenda likahitaji matengenezo ya mara kwa mara; upotevu wa nafaka mkubwa kuliko lile la kudumu kwa sababu ya ugumu wa kudhibiti wadudu na wanyama waharibifu.

- Ghala la kudumu [*liliotengenezwa kwa tofali na saruji*]. Hili hudumu kipindi kirefu, lakini ni gharama kulitengeneza. Faida yake ni kudhibiti upotevu utokanao na wadudu na wanyama waharibifu.

Benki Mazao katika hatua za mwisho za ujenzi

Ndani ya mojawapo ya Benki Mazao

- Ghala la kukodi au kuazima: Hili linaweza kuwa na gharama nafuu, isipokuwa wasiwasi ni mwenye mali kubadilika kwa kuhitaji jengo lake au kufanya mabadiliko ya pango bila utaratibu mzuri hii inaweza kupelekea hasara, uharibifu au matatizo mengine.

Mfano wa jengo lililoazimwa kwa lengo la kukarabatiwa katika kijiji cha Chifutuka, Wilaya ya Dodoma vijijini kwa ajili ya kuhifadhi nafaka kwa mfumo wa Benki Mazao

Maeneo mengi ambayo jamii zimehamasika kuanzisha mfumo wa Benki kama hizi, kumekuwa na dhana kuwa hatua ya mwanzo katika uanzishaji wa aina hizi za taasisi, msingi mkuu ni kuwa na jengo. Inawezekana kuwa sahihi katika vipindi na mazingira tofauti. Lakini ni vema jamii ikajikita zaidi katika kiini cha uanzishaji hasa pale ambapo jamii imeweza kutambua visababishi na athari za upungufu au ukosefu wa chakula, mbegu na masoko duni ya mazao ya wakulima.

Mihimili mikuu ya uanzishwaji wa Benki Mazao inaweza kuwa pamoja na :

Kwa kiasi kikubwa Benki Mazao inabebwa na WAZO la kuwa na akiba kwa njia ya mazao kwa upande mmoja. Kwa upande mwingine ni muhimu pia kuwa na badiliko la TABIA lililojengeka katika msingi wa kujiwekea akiba ili utumie baadaye wakati wa upungufu au unapokuwa na HITAJI.

Hivyo basi utekelezaji wa MAWAZO mazuri ya kuanzisha benki za namna hii unaweza kufanyika bila kusubiri ujenzi wa jengo maalum la Benki Mazao. Pamoja na jengo kuwa na umuhimu wa pekee katika shughuli hii, bado linaweza kujengwa baada ya wahusika kupata uwezo wa kufanya hivyo bila kusitisha hatua ya kutekeleza wazo la msingi kwa kutumia nyenzo zilizopo. Maana Palipo na Nia Pana Njia.

HATUA YA SITA
UAMUZI WA KUANZISHWA KWA MFUKO WA JAMII NDANI YA BENKI MAZAO:

Benki inaweza kuanzisha mfuko wa jamii *k.m. unaweza kuweka utaratibu kuwa, kila mtu anayenunua mazao/nafaka anachangia kiasi kidogo kwa ajili ya mfuko wa jamii* ambao unalenga kusaidia makundi yasiyo na uwezo [*kwa sababu mbali mbali*] ndani ya jamii.

SEHEMU YA TATU
JINSI BENKI MAZAO ZINAVYOFANYA KAZI [UTENDAJI NA USIMAMIZI]

Uzoefu wa uendeshaji wa Benki Mazao toka Tarafa ya Chilonwa, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma :

MIKAKATI YA KUENDESHA BENKI MAZAO:

Kwa ujumla, vikundi au jumuiya hizi za wananchi zimefanya jitihada kubwa za kuanzisha vyombo vya aina hii. Utayari wao kushirikisha uzoefu walionao utakuwa faida kwa jumuiya nyingine nyingi. Ili kuthamini na kutunza kazi hii nzuri waliyoianza, ni vema Benki Mazao zikawa na mtiririko wa utaratibu na mikakati ifuatayo inayokusudia kuhakikisha ufanisi wa shughuli zao.

MATUMIZI YA MFUKO WA MZUNGUKO:

Mfuko huu umekuwa ukitumika kama sehemu ya MTAJI kwa ajili ya kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo, kununulia nafaka kutoka kwa wakulima wengine na kukopesha wafanyabiashara wadogo wadogo ndani ya jamii husika.

Mambo ya kuzingatia katika makubaliano ya mkopo ni pamoja na:

- Kuainisha aina za mikopo.
- Dhamana
- Viwango vya riba ya mkopo.
- Muda wa kurejesha mkopo.
- Ni mara ngapi mteja anaweza kukopa ndani ya msimu mmoja.
- Kuonyesha kama marejesho yanaweza kufanyika kwa fedha au vitu/mazao.
- Hatua zitakazochukuliwa iwapo mkopo hautarejeshwa au kucheleweshwa n.k..

Mikataba ya mikopo baina ya Benki Mazao na wanachama inaweza kutumia uzoefu wa taratibu zilizokuwa zikitumika katika ngazi za vikundi na kupata ushauri wa kutosha kutoka kwa taasisi/mashirika yenye utaalam huu.

AKIBA YA CHAKULA

Lengo la akiba hii ni kutoa nafasi kwa wananchi kutunza kiasi cha chakula ambacho kinaweza kutosheleza kipindi cha upungufu kwa eneo husika.Kila mwanachama analazimika kutunza angalau gunia moja (Kilo 120) la nafaka. Wasio wanachama wana hiari ya kutunza kiasi wanachotaka katika akiba hii kutegemeana na ukubwa wa ghala.

Kipindi cha kuhifadhi kitakuwa ni muda wa kutosha baada ya kuvuna ili kuruhusu unyevu wa nafaka hizo kushuka kufikia kiwango ambacho kitaruhusu hifadhi bila uharibifu utokanao na kutokauka vizuri. Wanachama wataruhusiwa kuchukua chakula katika awamu au vipindi vitatu ambavyo ndivyo vina upungufu na umuhumu zaidi wa chakula (kwa maana ya kumwezesha mhusika kulima shambani kwake badala ya kufanya vibarua vya kutafutia chakula). Atakayetunza nafaka yake atatakiwa kulipa debe moja (Kilo 20) kwa kila gunia litakalotunzwa katika Benki kama gharama za utunzaji. Gharama za hifadhi kwa wale ambao si wananchama zitakuwa juu kidogo ya zile za wanachama.

AKIBA YA MBEGU:

Hii ni kwa ajili ya kuwahakikishia wanachama kuwa kila msimu wanakuwa na kiasi cha mbegu ya kuwatosha kutokana na kuchagua kutoka mavuno yao ya msimu uliopita au mbegu bora ya kununua. Katika akiba ya mbegu, kila mwanachama anatunza angalau kilo 20 za mbegu bora.

Mbegu zitaandikwa majina ya wenye mali. Mbegu zitatiwa dawa na kuhifadhiwa vizuri ili kudhibiti wadudu waharibifu na kuhakikisha uotaji wake msimu unaofuata. Wanachama wataruhusiwa kuchukua mbegu siku chache kabla ya msimu wa kupanda kuanza. Mwanachama hatatozwa gharama za utunzaji wa mbegu ndani ya benki.

AKIBA YA KAWAIDA AU YA KUMUDU SOKO:

Akiba hii inatoa fursa kwa wanachama na wasio wanachama kupata hifadhi bora na salama ya mazao yao. Pia akiba hii inawasaidia wateja wasiuze mazao yao kwa hasara [**yaani mapema sana mara baada ya kuvuna bei inapokuwa chini sana**]. Kwa lugha nyingine akiba hii ni mkakati wa soko ambao unalenga kuuza chakula kipindi ambacho bei inakuwa imepanda au inakuwa ya kuridhisha. Hapa Benki inahusika na taratibu zote za hifadhi bora ikiwemo kupiga dawa mazao yote ya wawekaji. Mazao yatatunzwa kwa kipindi angalau cha miezi mitatu (Julai hadi Septemba – Uzoefu wa Benki mazao maeneo ya Dodoma). Mwekaji atalipa gharama zote za utunzaji kama kawaida. Wanachama na wasio wanachama watawajibika katika kuuza mazao yao wenyewe. Benki itahusika katika kuingia makubaliano na wanunuzi ili mazao yanunuliwe yote kwa mkupuo na kwa bei inayomsaidia mteja wake (wakulima).

MIKOPO YA FEDHA KWA WANACHAMA:

Benki itatoa mikopo kwa wanachama ambao wamehifadhi mazao yao ndani ya Benki kama dhamana (Akiba ya Kawaida), hasa katika kipindi ambacho bei ya mazao iko chini sana. Mikopo ya fedha itatolewa pale ambapo bei ya mazao si ya kuridhisha. Riba ya mkopo italipwa kwa fedha taslimu mara baada ya kuuza mazao.

MKOPO WA CHAKULA:

Mikopo ya chakula hutolewa katika kipindi cha upungufu ambacho hudumu kwa takribani miezi mitatu. Aina hii ya mkopo hutolewa kwa wanachama tu.

Masharti ya mkopo huu ni:

Mkopo hutolewa kwa wanachama ambao wana uzalishaji wa kuridhisha, unaowawezesha kurejesha. Riba ya mkopo huu ni 50% ya mkopo uliochukuliwa. Yaani ukikopa gunia moja unarejesha gunia moja na nusu. Marejesho ni kwa njia ya mazao tu, si fedha. Kipindi cha marejesho ni Agosti (au msimu wa mavuno). Mkopo huu ni kwa ajili ya chakula hivyo mkopaji haruhusiwi kabisa kuuza mkopo huu.

Ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa taasisi kama Benki Mazao, ni muhimu kutambua aina na kiwango kinachohitajika na wanachama au wanajamii katika kipindi cha upungufu au njaa kabla ya kuanza kufikiria kutoa huduma.

Ununuzi wa nafaka/mazao

Kama Benki ina mtaji inaweza kununua mazao au nafaka wakati wa mavuno kwa sababu bei za mazao huwa chini kidogo. Ni vema kuanza kununua kutoka kwa wanachama, baadaye wanajamii wengine na hatimaye kwa wachuuzi au Benki jirani. “Bei ya kununulia kwa wanachama au wanajamii inaweza kuwa ya juu kuliko ile iliyopo sokoni, lakini inaponunua toka kwa wachuuzi isizidi bei ya soko kwa wakati huo”. Kiwango cha kununua kitegemee mahitaji ya wanachama au wanajamii katika kipindi cha upungufu wa chakula au njaa ambayo huidhinishwa mapema kabla. Lakini hii pia hutegemea kiasi cha fedha kilichopo.

Uuzaji wa nafaka/mazao

Wanachama wa Benki Mazao ndio wanaotakiwa kutoa maamuzi juu ya lini mazao yaanze kuuzwa. Ni lazima waamue kama ni kuuza msimu mzima au kipindi cha njaa/upungufu. Mara nyingi mauzo hufanyika wakati wa upungufu wa chakula au njaa wakati ambapo

watu wengi wamemaliza akiba zao za chakula na ni vigumu kwao kumudu gharama ya ununuzi wa chakula katika soko la kawaida. Lakini hii itategemea utashi wa Benki. Inawezekana Benki ikauza msimu mzima kwa kuendelea kurudishia akiba kila inapoisha. Hii hutokea zaidi katika maeneo ambayo uzalishaji uko chini au hautoshelezi au kwenye maeneo ya wafugaji ambao hawalimi kabisa. **"Hata hivyo kutoa huduma kwa mwaka mzima kunahitaji uongozi makini sana".**

Kwa mtindo huu, Benki huanza kuuza mazao kwa wanachama wake na baadaye kwa wasio wanachama [kama wamejitosheleza]. Kwa kawaida wanachama huuziwa kwa bei nafuu kuliko wasio wanachama. Hapa ni vema kuangalia mahusiano ya bei ya kuuzia kwa kuzingatia gharama halisi za utunzaji wa nafaka.

Msaada kwa wasio na uwezo

Kila inapojitokeza upungufu au njaa, kila mmoja ataangalia Benki Mazao kama mkombozi na kutaka kununua chakula. Hapa izingatiwe kuwa baadhi ya wanajamii wana uwezo zaidi ya wengine, na wenye uwezo wanaweza kutaka kununua zaidi au hifadhi yote bila kufikiria wengine. Katika hali hii, ni vema Benki ikawa na taratibu na mifumo itakayosimamia ununuzi na uuzaji wa chakula, vinginevyo makundi yasiyo na uwezo hayatanufaika na uwepo wa Benki katika eneo lao.
Baadhi ya mbinu zinazoweza kutumika katika kusaidia makundi yasiyo na uwezo ni pamoja na:

- Kuweka kiwango ambacho kitaruhusiwa kwa kila mwanajamii bila kujali hadhi yake n.k;
- Kufahamu mahitaji halisi ya familia na kiwango wanachotaka kununua *k.m. Benki inaweza kuamua kuwa, kila kiongozi wa kaya anaruhusiwa kununua kiwango kisichozidi kilo 100 kila baada ya wiki mbili*. Hii pia huzuia mtu kununua kiwango kikubwa na kukiuza kwa kutengeneza faida au kusababisha wengine kutopata huduma ya kutosha;
- Kutoa mikopo: hapa Benki inaweza kuweka utaratibu wa kununua kwa mkopo. Kabla ya kufanya hivyo, ni vema Benki ikajiridhisha katika mambo yafuatayo:

- ⇨ Ni watu wangapi wanaweza kuhitaji mkopo?
- ⇨ Kiasi gani cha nafaka kilichopo ghalani ambacho kinaweza kutolewa kwa mkopo?
- ⇨ Ni njia ipi itatumika kudhibiti ukwepaji wa kulipa mkopo au kudhibiti wadaiwa/madeni?

SEHEMU YA NNE
MATOKEO CHANYA YA UANZISHWAJI WA BENKI MAZAO *UZOEFU KUTOKA KATIKA TARAFA YA CHILONWA – DODOMA*

- Mpaka kukamilika kwa Programu ya Uhakika wa Chakula, jumla ya ya majengo 13 [Kama Benki za Mazao] katika tarafa ya Chilonwa, Gairo na Mikese] yalikuwa yamejengwa. Majengo hayo yamejengwa kwa michango mbalimbali ikiwemo ya Serikali za vijiji kwa kutoa viwanja, Wananchi kutoa nguvu kazi wakati wa ujenzi na Mradi kutoa vifaa vya ujenzi;
- Wakati wa ujenzi, uzoefu wa Chitego ulitumiwa kwa sehemu kubwa. Kwa wastani, kila jengo lina uwezo wa kuhifadhi magunia elfu moja YA KILO MIA MOJA kwa wakati mmoja;
- Kiwango cha usalama wa mazao yaliyohifadhiwa kiliongezeka kati ya 50% - 70%. Kwa maana ya kuwa uharibifu wa mazao ghalani ulipungua kwa kiasi kikubwa;
- Hifadhi ya akiba na mikopo ya chakula wakati wa kilimo imewawezesha wananchi wengi kulima mashamba yao badala ya kwenda kufanya vibarua kama ilivyokuwa awali. Hii imepunguza sana uhaba wa chakula kwa kaya nyingi kutokana na ongezeko katika uzalishaji wa chakula;
- Pale ambapo Benki hizi zimefanya shughuli zake kwa ufanisi, ukiacha kutosheleza wanachama kwa chakula, lakini pia Benki hizi zimeweza kuhudumia hata wale ambao si wanachama. Kuhudumia makundi maalum *k.m. wazee, waathirika, wajane n.k.* Wakulima wameweza kupata bei nzuri kwa mazao yao kupitia akiba;
- Kwa kiwango cha kuridhisha, athari mbaya zitokanazo na upungufu au ukosefu wa chakula zimepungua *k.m. kuzikimbia familia, kuuza nguvu kazi [kufanya vibarua] n.k;*
- Mwamko wa wananchi kupanga matumizi yao ya chakula na kutumia Benki Mazao kuweka akiba ya kutumia wakati wa kilimo umeongezeka katika maeneo ya mradi. Mfano benki ya Chitego haiwezi tena kumudu kikamilifu mahitaji ya jamii ya kuhifadhi nafaka kwani nafaka inayohitajika kuhifadhiwa ni nyingi kuliko uwezo wa benki;
- Wanavikundi wameelewa umuhimu wa kutoa hisa zao kwa ajili ya Benki Mazao. Mfano, kwa vijiji vya Mgunga na Mnase kila mwanakikundi anatoa Debe 3; Makoja, Chitego, Manchali na Chalinze kila mwanachama anatoa gunia 1 kama hisa;

- Ongezeko la uzalishaji mazao kwa kiwango cha hadi 40% kwa baadhi ya maeneo na walengwa kutegemeana na hali ya hewa pamoja na uzingatiaji wao wa kuweka mafunzo katika vitendo;
- Mikopo ya fedha kwa dhamana ya nafaka imewezesha baadhi ya wakulima (waliohifadhi nafaka zao za ziada katika benki mwaka 2004), kufanikiwa kuuza nafaka kwa bei ya sh. 27,000/= kwa gunia badala ya sh. 8,000/=. Mkopo wa fedha walioupata kutoka benki mazao uliwasaidia wakulima kusubiria bei nzuri ya kuuzia mazao yao;
- Vikundi au wanavikundi wameweza kubuni na kuendesha miradi midogo midogo ya kiuchumi k.m ufugaji, maduka, mashamba ya pamoja, bustani za mboga mboga n.k.

Ushuhuda 1: Mkulima Leonard Nyanda wa Kijiji cha Chitego aliandika makala katika Jarida la Kilimo Endelevu [Toleo namba 8 – July – Agosti 2006] anaona manufaa ya Benki Mazao kuwa ni pamoja na:

- *Tatizo la njaa kupungua kwa 80% katika kijiji cha Chitego;*
- *Mtaji wa Benki kukua kutoka magunia 36 mwaka 1999 hadi magunia 420 mwaka 2004;*
- *Uhakika wa upatikanaji wa mikopo ya chakula na uzalishaji kwa riba nafuu;*
- *Kuambukiza uzoefu katika maeneo mengine ya nchi k.m. vijiji vya Majawanga na Mkalama [Gairo]; Fulwe na Newland [Morogoro vijijini]; Makoja, Chalinze, Manchali, Chinangali, Mgunga, Mnase na Mlebe [Chamwino].*

Ushuhuda 2: Mkulima Stephano Sabugo wa kijiji cha Makoja – wilaya ya Chamwino aliandika makala katika gazeti la Ground Up [Volume 1 No 13] akielezea pamoja na manufaa yaliyotajwa hapo juu ya Benki Mazao [Kuweka na kukopa mazao], lakini benki hizo pia ziliweza kukopesha pembejeo na zana za kilimo k.m majembe ya kukokotwa na ng'ombe, mikokoteni, haro na zana za kupalilia. Hizi zililenga kurahisisha shughuli za kilimo na kuwahi msimu wa kilimo kinyume na kutumia jembe la mkono.

Mkopaji wa zana na pembejeo, hutakiwa kuwa na dhamana ya akiba ya nafaka [Chakula] katika Benki Mazao ambayo inalingana na asilimia 60 ya thamani ya mkopo. Asilimia 40 inayobaki italipwa baada ya kuuza mazao yaliyohifadhiwa kwa bei ya juu na kama haitoshelezi malipo hufanyika msimu ufuatao wa mavuno.

SEHEMU YA TANO
CHANGAMOTO ZA UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA BENKI MAZAO:

Kama ilivyo kwa taasisi nyingine zilizojikita katika utoaji wa huduma kwa jamii, Benki Mazao pia zinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Benki Mazao zinakabiliwa na changamoto kuu mbili:

CHANGAMOTO ZA NDANI

- Benki Mazao kuweza kuhudumia kwa utoshelevu mahitaji ya jamii pana [hasa makundi maalumu] badala ya uwezo wa sasa kuhudumia sehemu tu ya wana jamii [wanachama au wanakikundi];
- Kuweza kubaini na kupata Uongozi makini [Stadi, Maarifa, Umahiri, Uaminifu na Uadilifu] ambao utabeba dhamana ya kukiendesha chombo kwa mtazamo chanya wa kuhudumia jamii kwa kiwango bora na cha kutosheleza;
- Kumudu na kuchukua chachu zinazotokana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ndani ya jamii husika [Hivyo kuathiri mshikamano au malengo ya kikundi] kama sehemu muhimu ya kuboresha utoaji huduma katika taasisi hizi;
- Kujenga nguvu za ushawishi na utetezi kwa jamii, serikali na wadau wengine ili kuunga mkono dhamira ya uanzishwaji, uendeshaji na manufaa ya taasisi kama Benki Mazao katika mifumo ya sera na sheria;
- Kuwezesha jamii kuwa bunifu katika kuwa na vyanzo mbadala vya kipato ili kuepuka kutegemea mazao ya chakula kama chanzo cha mapato [Rejea hali halisi ya mikoa kame kama vile Dodoma];
- Kubadilisha mazoea na mtazamo wa wakulima katika sekta ya kilimo ili waweze kutumia mbinu bora za kilimo ili kukifanya kilimo kuwa shughuli yenye tija.

CHANGAMOTO ZA NJE

- Mabadiliko ya Tabia nchi ambayo yamesababisha kupungua kwa uzalishaji na hivyo kuathiri uwezo wa wakulima katika kuweka akiba ya mazao lakini pia kushindwa kufanya marejesho ya mikopo ndani ya Benki Mazao;
- Uwezo mdogo au ukosefu wa mitaji ya kuwekeza kwenye kilimo hasa kwa wakulima wadogo wadogo, hivyo kuishia katika matumizi madogo ya pembejeo na zana duni ambazo haziongezi tija;
- Mifumo na sera kutolinda vya kutosha maslahi ya mkulima katika mnyororo wa uzalishaji mpaka masoko ya wakulima wadogo wadogo hapa nchini.

SEHEMU YA SITA
UENDELEVU WA BENKI MAZAO

Pamoja na jitihada na matokeo chanya ya uwepo wa taasisi za utoaji huduma katika eneo la Uhakika wa Chakula, ni vema jamii iliyojikita katika mfumo huu kujiwekea mikakati ya kupambana na changamoto zinazojitokeza na kulinda manufaa yatokanayo na jitihada hizo. Baadhi ya misingi muhimu katika kuhakikisha uendelevu wa Benki Mazao ni pamoja na:

- Taasisi hizi kuwa na Mwelekeo [Dira] na mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu inayotekelezeka, kukubalika na kuheshimika kwa wanachama na wanufaikaji wengine;
    - Benki kutengeneza mifumo, taratibu na miongozo inayoelekeza utoaji huduma bora na za kutosha kwa makundi mbali mbali yanayonufaika na huduma za taasisi hii
- Kuhakikisha kwamba wadau wote wanaochangia na wanaonufaika na huduma za Benki mazao wana mahusiano thabiti na yanayochangia ufanisi wa utoaji huduma. Ni vema kuongoza kwa vitendo masuala yanayogusa Uwazi, Ushirikishwaji na Uwajibikaji ndani ya Taasisi kama chombo cha wanachama;
- Benki kujenga mahusiano yenye tija na taasisi au makundi yenye mwelekeo kama wao ili kuweza kupambana na changamoto zinazohitaji nguvu ya pamoja
    - Benki zisajiliwe kisheria ili kuweza kuwa na sauti katika masuala yanayohusu maslahi ya wenye benki hizo kwa faida yao na jamii inayowazunguka;
    - Hii pia itasaidia kutambulika na kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya nchi na itaongeza fursa ya kushirikiana na wadau wengine katika nyanja za maendeleo.
- Benki ziwe na mahusiano au ushirikiano na Taasisi nyingine kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi zake. Izingatiwe kuwa mahusiano haya yasiathiri mtazamo au mwelekeo wa Benki hizo.

HITIMISHO

Ndugu mtumiaji wa kijitabu hiki, ni matarajio ya watayarishaji kuwa umejifunza mengi na kwamba mafunzo ndani ya kijitabu hiki yanaweza kuwa msingi na chachu ya kupata mbinu bora zaidi ya kupambana na upungufu au ukosefu wa chakula kuanzia ngazi ya kaya mpaka jamii kwa ujumla.

Pamoja na jitihada zilizoongelewa ndani ya kijitabu hiki, baadhi ya mambo makuu yanayoweza kuwa yamejitokeza ni pamoja na:

- Kwamba: athari za Upungufu au Ukosefu wa chakula zinaweza kudhibitiwa au kupunguzwa kwa kutumia mfumo huu au mwingine unaofanana na huu;
- Kwamba: Mpaka pale jamii itakapotambua kiini cha athari za upungufu au ukosefu wa chakula na kutoa vipaumbele, ndipo jitihada thabiti za kupunguza tatizo hilo zitafanyika na kuhakikisha uendelevu wa jitihada za kudhibiti;
- Kwamba: Ni vema jamii ikawezeshwa kumiliki mchakato wa uanzishwaji, uendeshaji na matokeo ya kuwepo kwa Benki Mazao kama sehemu ya uendelevu;
- Kwamba: Taasisi au mashirika nje ya jamii iliyo/ inayoathirika yabaki kuwa “Wawezeshaji” na jamii kuwa ‘Wachezaji halisi” wa mchakato ili kupunguza utegemezi na hivyo kuongeza umiliki.

Benki Mazao ni thibitisho la uhakika wa chakula kwa jamii za wakulima wadogo vijijini.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mratibu,
PELUM Tanzania
S.L.P 390,
Morogoro Tanzania
Simu/Nukushi: +255 23 2613677
Barua Pepe: info@pelumtanzania.org
Tovuti: www.pelumtanzania.org